

Muhtasari kwa Lugha Rahisi wa Sera ya Msaada wa Kifedha wa Hospitali ya Watoto ya Dayton

Sambamba na dhamira yake ya kutoa huduma ya matibabu ya kina na uelewa ambayo inaboresha afya ya watu tunaowahudumia, Hospitali ya Watoto ya Dayton imejitolea kutoa Msaada wa Kifedha kwa kila mtu anayehitaji matibabu ya dharura au matibabu mengine muhimu ya kiafya ikiwa mtu huyo hana bima, ana bima isiyotosha, hastahiki kwa mipango mingine ya serikali, au ameshindwa kulipa kulingana na hali yake ya kifedha.

Matibabu Yanayostahiki.

Msaada wa Kifedha unapatikana chini ya Sera yetu ya Msaada wa Kifedha (FAP) kwa huduma ya matibabu ya dharura au matibabu mengine muhimu yanayotolewa na Hospitali ya Watoto ya Dayton kwa Wagonjwa Wanaostahiki.

Mahitaji ya Ustahiki wa Mgonjwa.

Mpango wa Msaada wa Kifedha wa Hospitali ya Watoto ya Dayton unapatikana kwa wagonjwa wasio na bima na wagonjwa walio na masalio ya kujilipia wenyewe baada ya bima ambao wamekidhi vigezo vyote vya kifedha kulingana na ufichuzi wa, na tathmini ya, maelezo na hati zinazofaa (Wagonjwa Wanaostahiki). FAP ni mpango wa hisani kulingana na mapato ya familia ya mgonjwa. Wagonjwa walio na mapato ya familia yanayolingana na au chini ya 400% ya Mwongozo wa Umaskini wa Nchi (FPG) wanastahiki msaada wa kifedha kwa kipimo kifuatacho cha uwezo:

KIWANGO CHA MAPATO

Mapato \leq 100% FPG
Mapato $>100\%$ na $\leq 200\%$ FPG
Mapato $>200\%$ na $\leq 300\%$ FPG
Mapato $>300\%$ na $\leq 400\%$ FPG

% YA PUNGUZO LA BEI

Msaada wa 100%
Msaada wa 80%
Msaada wa 60%
Msaada wa 15%

Msaada kwa COVID-19: Pamoja na taarifa iliyo hapo juu, kwa huduma za matibabu zilizotolewa kuanzia kipindi cha Aprili 2020 hadi Juni 2021, Dayton Children huenda ikatoa ustahiki kwa wagonjwa ili wapate punguzo la ziada la COVID-19 la msaada wa kifedha kwenye masalio ambayo hayajalipwa na mgonjwa. Ili kustahiki punguzo hili la bei, mgonjwa/familia lazima itume ombi la msaada wa kifedha kupitia mchakato wa kawaida kama ilivyoainishwa katika sera hii. Hatua ya kukamilika kwa mchakato huu wa maombi itatoa ustahiki kwa mgonjwa/familia, wakati huo, kwa punguzo la bei kwenye masalio ambayo hayajalipwa. Punguzo hili la bei litaanza kutumika kwa hiari ya Hospitali ya Watoto ya Dayton kwa muda unaohusiana na athari ya COVID-19 kwa jamii ya eneo la Dayton.

Wagonjwa walio na mapato ya familia yanayozidi 400% ya Miongozo ya Umaskini ya Nchi bado wanaweza kustahiki msaada wa kifedha kulingana na hali binafsi. Gharama na dhima ya Wagonjwa huzingatiwa katika tathmini ya ustahiki wao kwa uidhinishaji. Wagonjwa wanatarajiwa kuchangia malipo ya matibabu kulingana na hali zao za kifedha; kwa hivyo, kila hali itakaguliwa kivyake. Msaada wa Kifedha hauchukuliwi kama njia mbadala ya malipo na wagonjwa wanaweza kusaidiwa kupata njia nyingine za malipo au za msaada wa kifedha kabla ya kuidhinishwa kwa Mpango wa Msaada wa Kifedha wa Hospitali ya Watoto ya Dayton.

Hakuna Mgonjwa Anayestahiki atakayelipishwa zaidi kwa huduma ya matibabu ya dharura au huduma nyingine muhimu ya matibabu kuliko Gharama Zinazotozwa kwa Kawaida (AGB) kwa wagonjwa ambao wana bima inayoshughulikia matibabu hayo.

Kuhusu Mchakato wa Kutuma Maombi.

Mchakato wa kutuma maombi ya msaada wa kifedha chini ya FAP yetu unajumuisha hatua hizi:

1. Jaza Fomu yetu ya Maombi ya FAP (pia inajulikana kama FAA) na ujumuishe hati zinazofaa na zinazohitajika
2. Maombi yaliyojazwa yanaweza kurereshwa kwa njia zifuatazo: Tuma barua kwa: Hospitali ya Watoto ya Dayton, Wakili wa Kifedha wa Mgonjwa na Familia, Department 1A, One Children's Plaza, Dayton, Ohio 45404-1815 au kupitia faksi kwa: 937-641-6101 Makini kwa: Wakili wa Kifedha au kupitia barua pepe FinancialAdvocates@childrensdayton.org
3. Idara ya Msaada wa Kifedha itakagua maombi uliyojaza pamoja na hati ulizotoa ili kuamua ustahiki wako.
4. Tutawasiliana nawe iwapo maelezo zaidi yanahitajika ili kukamilisha mchakato wako wa maombi na/au wakati uamuzi umefanywa. Tafadhali tupe siku 30 ili kukamilisha mchakato wa tathmini.

Mahali pa Kupata Maelezo.

Unaweza kupata nakala isiyolipishwa ya FAP na Fomu yetu ya Maombi ya FAP kwa kutembelea tovuti yetu katika http://www.childrensdayton.org/cms/our_services/index.html au kwa kuwasiliana na Idara yetu ya Msaada wa Kifedha katika 937-641-3555. Baada ya ombi lako, Idara yetu ya Msaada wa Kifedha itakutumia nakala isiyolipishwa ya FAP yetu, Fomu ya Maombi ya FAP, na Muhtasari kwa Lugha Rahisi kwa anwani unayotupa. Nakala zisizolipishwa za FAP, Fomu ya Maombi ya FAP na Muhtasari huu wa Lugha Rahisi zinapatikana katika nakala halisi katika Hospitali ya Watoto ya Dayton, Idara ya Matukio ya Mgonjwa, One Children's Plaza, na Dayton, Ohio 45404.

Huduma nyingine ambazo zinatozwa kando na watoa huduma wengine ambao sio wafanyakazi wa Hospitali ya Watoto ya Dayton, kama vile madakatari huru, hazistahiki chini ya FAP yetu.

FAP yetu, Fomu ya Maombi ya FAP na Muhtasari kwa Lugha Rahisi zinapatikana kwa lugha za Kiingereza, Kihispania na Kirusi.